KANISA LA UINJILISTI TANZANIA
HOSPITALI YA MBALIZI - IFISI
(Umtumikie Mungu na Kuwahudumia Watu)
S.L.P 6117, MBEYA - TANZANIA (E.A)
SIMU: +255 674 551 110 // +255 767 554 844 // +255 714 542 568
www.mec.tanzania.ch mbalizihospital@gmail.com

**Kumb. Na.TEC/MH/GC/NH/03/26** **12 /02/ 2026**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Hospitali ya Mbalizi-Ifisi ipo kilometa 20, Magharibi mwa mji wa Mbeya pembezoni mwa barabara kuu ya Tunduma kwenda Zambia, nje kidogo ya mji mdogo wa Mbalizi, katika kijiji cha Ikumbi Ifisi.

Mbalizi Hospitali imepokea kibali cha ajira mpya kutoka kwa katibu mkuu wa Kanisa la Uinjilisti Tanzania kupitia **Kumb.Na. MH/GC/TEC/01/2025**. Ili kuajiri watanzania wenye sifa za kuajiriwa katika utumishi chini ya Kanisa la Uinjilisti Tanzania katika nafasi mbalimbali. Nafasi hizi ni mubadala (replacement) wa watumishi walioondoka.

Kwa madhumuni ya kuhakikisha Watanzania watakao ajiriwa wawe wenye sifa zinazotakiwa waombaji wanatakiwa kuzingatia sifa na vigezo kwa kila nafasi kama ilivyoainishwa hapo chini kama ifuatavyo:-

## 1. DAKTARI (Medical Doctor II) – (Nafasi 3)

### A) SIFA

Awe na shahada ya udaktari kutoka chuo/vyuo vinavyotambuliwa na Serikali. Awe amehitimu mafunzo ya vitendo "Internship".

Awe na usajili kutoka baraza la madaktari Tanganyika (medical council of Tanyangika).

### B) Kazi na Majukumu

i. Kufanya kazi zote za matibabu hospitalini zinazohusiana na magonjwa mbalimbali yakiwemo magonjwa ya Watoto, magonjwa ya akina mama na upasuaji wa kawaida na wa dharura.
ii. Kutao na kusimamia elimu ya afya pamoja na kuboresha afya ya jamii katika Wilaya na Mikoa au eneo lake la kazi.
iii. Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa.
iv. Kutunza takwimu na kuzitumia kama inavyoelekezwa katika misingi ya MTUHA.
v. Kupanga na kutathimini huduma za afya katika eneo lake la kazi.
vi. Kufundisha wanafunzi na watumishi waliopo kwenye eneo la kazi
vii. Kusimamia na kuendekeza wafanyakazi walio chini yake.
viii. Kufundisha wanafunzi katika vyuo vya afya vilivyopo eneo lake la kazi.
ix. Kubuni na kuendesha utafiti na kusambaza matokeo
x. Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma ya fani yake.

xi. Kuandaa mipango na makisio ya bajeti ya huduma za afya
xii. Kushiriki, kuhakiki na kuboresha huduma za afya (medical audit and quality improvement)
xiii. Kutoa huduma za outreach katika Wilaya/mkoa wake
xiv. Kufanya kazi nyingine atazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**Mshahara:-**
*Ataanza na ngazi ya mshahara wa* ***TGHS E***

**2. DAKTARI BINGWA WA UPASUAJI (GENERAL SURGEON) nafasi 1**

**A) SIFA**
Awe na shahada ya uzamili ya udaktari Bingwa wa upasuaji (surgeon) (M.Med kwenye fani ya udaktari) ya miaka mitatu au zaidi kutoka vyuo vikuu vinavyotambuliwa na serikali.

Awe amesajiliwa na baraza la madaktari (medical council of Tanganyika)

**B) KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kuona wagonjwa wote wenye matatizo ya upasuaji, kufanya uchunguzi wa kina ili kutambua kama mgonjwa anatatizo linalohitaji upasuaji au la
ii. Kuamua aina ya upasuaji, kumweleza mgonjwa aina hiyo ya upasuaji ikiwa ni pamoja na kuandaa matibabu ya kabla ya upasuaji.
iii. Kufanya upasuaji wa matatizo yote yanayo hitaji upasuaji kwa kutumia vifaa kwa ustadi na umakini.
iv. Kusimamia timu ya chumba cha upasuaji na kuwa kiunganishi kati ya wodi ya upasuaji na na timu ya chumba cha upasuaji.
v. Kupanga ratiba ya upasuaji na kuanda orodha ya wagonjwa (list) siku moja kabla ya upasuaji.
vi. Kufuatilia hali ya wagonjwa baada ya upasuaji, kuhakikisha anapata dawa za maumivu na kuzuia maambukizi au matatizo yanayoweza kujitokeza baada ya upasuaji.
vii. Kushauri wagonjwa na ndugu wa wagonjwa kuhusu utunzaji wa kidonda, ratiba ya kusafisha na mabadiliko ya mtindo wa maisha baada ya upasuaji.
viii. Kufanya kazi kwa ushirikiano na madaktari wengine,wauguzi na wataalamu wa dawa za usingizi ili kumsaidia mgonjwa.
ix. Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na muajiri na msimamizi wake wa kazi.

**Mshahara:-**
Hospitali italipa mshahara kiwango zaidi ya kiwango cha serikali yaani zaidi ya **TGHS G.**

**3. DAKTARI BINGWA WA MAGONJWA YA NDANI (PHYSICIAN) nafasi 1**

**SIFA ZA MUOMBAJI**
Awe na shahada ya uzamili ya udaktari Bingwa wa magonjwa ya ndani (Physician) (M.Med kwenye fani ya udaktari) ya miaka mitatu au zaidi kutoka vyuo vikuu vinavyotambuliwa na serikali.

Awe amesajiliwa na baraza la madaktari (medical council of Tanganyika)

**KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kutambua na kutibu magonjwa ya ndani ya mwili kwa watu wazima bila kufanya upasuaji kushughulika na magonjwa ya viungo vya ndani kama moyo, mapafu, figo, ini, na mfumo wa mmeng'enyo wa chakula.
ii. Kufuatilia maendeleo ya wagonjwa wa muda mrefu kama ufuatiliaji wa vipimo kila baada ya muda fulani pamoja na kubadilisha matibabu pale inapo hitajika.
iii. Kutoa huduma za kinga yaani ushauri juu ya lishe na mtindo wa maisha, kutoa ushauri juu ya chanzo na namna ya kuzuia magonjwa sugu.
iv. Kusimamia matibabu ya wagonjwa waliopo wodini kwa kufuatilia hali zao kila siku na maendeleo ya matibabu.
v. Kusimamia kliniki za wagonjwa sugu wodi ya wagonjwa wasio wa upasuaji (Medical) pamoja na ICU.
vi. Kuratibu rufaa ya wagonjwa kwa wataalamu wengine kutokana na aina ya Tatizo alilo nalo mgonjwa mfano Daktari wa moyo, Daktari wa Figo au Upasuaji.
vii. Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na muajiri wake.

**Mshahara:-**

Hospitali italipa mshahara kiwango zaidi ya kiwango cha serikali yaani zaidi ya **TGHS G.**

**4. Mhasibu Daraja la II (ACCOUNTANT II) nafasi 1**

**A) SIFA**

i. Awe na elimu ya kidato cha nne au cha sita
ii. Awe na shahada ya Biashara/uhasibu kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali
iii. Awe na cheti cha taaluma ya uhasibu CPA (T) kinachotambuliwa na NBAA.
iv. Awe na ujuzi wa kutumia mifumo ya kiuhasibu kama quick book, pastel au mifumo mingine
v. Awe na uzoefu usiopungua miaka minne kufanya kazi katika sekta binafsi, mashirika au Asasi zisizo za kiserikali
vi. Awe mtanzania mwenye kitambulisho cha NIDA

**B) KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za taasisi kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kuandaa taarifa za mapato na matumizi kwa mujibu wa kanuni za fedha.
ii. Kupitisha malipo kulingana na sheria na kanuni za fedha.
iii. Kusi mamia uandaaji wa taarifa mbalimbali za mishahara.
iv. Kusimamia urejeshwaji wa masurufu kulingana na kanuni na taratibu za fedha.
v. Kufanya ukaguzi wa fedha katika idara anayosimamia ndani ya taasisi.
vi. Kutoa na kuandaa taarifa za makisio ya mapato na matumizi ya taasisi (bajeti) ya mwaka

vii. Kutoa ushauri na kutafsiri sheria na kanuni za fedha kwa uongozi wa Taasisi
viii. Kuandaa *cash flow statements*
ix. Kusimamia vyanzo vyote vya mapato ya taasisi na kuhakikisha mauzo yanafanyika kwa kufuata taratibu.
x. Kufanya usuluhisho wa hesabu za benki na nyingine zinazohusiana na masuala ya fedha.
xi. Kukagua hati za malipo
xii. Kufanya kazi nyingine za fani yake atakazopangiwa na mwajiri wake.

**MSHAHARA.**

Ngazi ya mshahara ni tofauti na serikali, yaani zaidi ya TGS E

**MAELEZO YA JUMLA**

- Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi 45.
- Waombaji waambatanishe wasifu binafsi (curriculum vitae) anuani inayotumika, namba ya simu na anuani ya barua pepe (e-mail address) na majina matatu ya wadhamini (referees) watatu.
- Waombaji waambatanishe cheti cha kidato cha nne, cheti kidato cha sita, cheti cha kuzaliwa, vyeti vya taaluma, leseni ya taaluma, cheti cha mafunzo ya internship (kwa madaktari).
- Matokeo ya muda (provisiona/testimonial/statement result) havitakubalika.
- Waombaji watakao wasilisha vyeti vya kughushi hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.
- Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne vya nje ya nchi vihakikiwe na vithibitishwe na baraza la mitihani Tanzania (NECTA).
- Barua ya maombi itatakiwa iandikwe kwa mkono kwa lugha ya Kiswahili au kiingereza.
- Waombaji waambatanishe kitambulisho cha uraia (national identification number) kinachotolewa na mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA).
- Kila barua ya muombaji iambatanishwe na picha mbili ndogo (passport size) iliyopigwa siku za karibuni, anuani kamili ya makazi pamoja na namba ya simu.
- Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta, barua au kwa kuwasilisha mkononi kwa ofisi ya katibu wa hospitali Teule ya Wilaya.
- Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na namba za simu za kuaminika. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 20/02/2026

Maombi yote yawasilishwe kwa anwani ifuatayo:-

Mganga Mfawidhi
Mbalizi Hospitali
S.L.P 6117
Mbeya

Au tuma kwa mbalizihospital@gmail.com CC faustinafn@gmail.com

Maulizo piga namba za simu zifuatazo 0674 551110